## 1. Utangulizi

1.1 Masharti haya yanaanza kutumika unapojisajili kwa ajili ya akaunti ya miamala ya biashara.

1.2 Sharti ujue, kuelewa na kutekeleza Maelezo ya Jumla na Masharti yake kwa kuwa ni mkataba rasmi kati yako na sisi.

1.3 Iwapo kuna mgongano kati ya maelezo haya na maelezo ya Jumla na Masharti, maelezo haya yatatumika.

1.4 Vipengele muhimu ambavyo vinaweza kupunguza mamlaka yetu au kukusababisha hatari. vitaandikwa kwa herufi kubwa. Sharti uwe na tahadhari na vipengele hivi.

## 2. Tafsiri

**Akaunti**: Akaunti ya Miamala ya Biashara iliyofunguliwa na sisi kwa jina lako na maombi yako.

**Benki, sisi:** Benki ya Stanbic Tanzania ( yenye Namba ya Usajili Na 22443) na waandamizi wake au wahawilishiwa.

**Kadi:** Kadi yoyote ya Benki tunayotoa kwako pamoja na Kadi ya ziada nyingine na kadi ya kubadilisha.

**PINI**: Namba ya siri ya utambulisho inayotumika kwa matumizi ya Akaunti yako.

**Wewe/Yako**: Ni mtu (pamoja na mtu kisheria) aanayeomba kufungua Akaunti, au ambaye akaunti inafunguliwa kwa jina lake na pamoja na waandamizi au wahawilishiwa wako.

## 3. Uwekaji

3.1 Kufungua Akaunti yako sharti ufanye malipo ya chini kabisa yanayotakiwa kwa ajili aya Akaunti yako.

3.2 Tutaridhia uhamishaji wa fedha kielektroniki, taslimu na hundi katika Akaunti yako.

3.3 Hutaweka hundi ya baadaye bila kupanga na tawi lako.

## 4. Kubadilishwa Uwekaji

4.1 Endapo hundi au kitu mfano wake iliyoingizwa kwenye Akaunti yako haikuweza kulipwa, tutakata Akaunti yako kwa kiwango kinachoainishwa katika hundi.

4.2 Endapo wewe sio mpokeaji halali wa hundi iliyoingizwa katika Akaunti yako, tunaweza kukata kutoka Akaunti yako kwa kiwango kilichoainishwa katika hundi na kuzilipa pesa kwa mpokeaji halali. Hata hivyo tutakutaarifu endapo tumefanya hivyo.

## 5. Malipo

5.1 Tutafanya malipo kwenye Akaunti yako endapo:
unatuelekeza kufanya hivyo.
na kuna fedha za kutosha kwenye Akaunti yako.

## 6. Kusitisha malipo

6.1 Unaweza kusitisha malipo ya hundi ambayo umeitoa kabla haijawasilishwa benki kwa malipo isipokuwa kama tumethibitisha kwamba tutalipa.

6.2 Unaweza kupinga na/au kusitisha malipo katika maelekezo yako ya makato kwa maandishi. Ni wajibu wako kumuarifu mtu anayetoa pesa kwenye Akaunti yako.

## 7. Maelezo

Tutakupa maelezo ya kila mara kuhusu Akaunti yako.

## 8. Kitabu cha Hundi

Unaridhia kuchukua na kutumia kitabu cha Hundi chochote na fomu zozote za hundi kwa ungalifu mkubwa.

8.1 Pia unakubali kuhakikisha:

8.1.1 fomu za hundi zote ambazo hazijakamilishwa zinawekwa sehemu salama wakati wote.

8.1.2 kwamba tuna taarifa mara moja baada ya wewe kugundua kitabu chochote cha hundi au fomu za hundi vimeibwa, kupotea au kutofahamika vilipo.

8.1.3 kwamba mtu yeyote anayeandaa hundi ameidhinishwa kufanya hivyo.

8.1.4 kwamba kila hundi imeandaliwa na kutiwa saini kwa wino au kitu kingine kisichofutika.

8.1.5 kwamba kiasi kinachoandikwa kwenye hundi kinakuwa katika hali ya kuzuia ongezeko lolote la maandishi au tarakimu ambalo halikuidhinishwa.

8.1.6 kwamba kila hundi au mabadiliko vinatiwa saini na mtiaji saini aliyeidhinishwa.

8.1.7 kwamba hakuna hundi ambayo haijakamilishwa inakabidhiwa kwa mtu asiyefahamika au mtu mwingine kama huna sababu za maana kuamini kwamba mtu huyo ni muaminifu.

8.1.8 kwamba baada ya kufungwa kwa Akaunti yoyote utarejesha kwetu fomu za hundi zozote zilizosalia ambazo hazijatumika mintarafu Akaunti hiyo na tutakurejeshea, inapowezekana, thamani za stempu za hazina kwa malipo yake ambazo tunazo.

8.1.9 kwamba unaelewa kuwa matumizi na uhifadhi wa kitabu chako cha hundi inategemea utaratibu tunaoweza kuwa nao mintarafu utekelezaji wa mfumo wa MICR ( Magnetic Ink Character Recognition) pamoja na ACH ( Automated Clearing House).

**9. Mkopo**

9.1 Ikiwa akaunti yako inakopwa bila utaratibu unaofaa, tunaweza kuhamisha pesa kwenye akaunti hiyo kutoka akaunti zako nyingine.

9.2 Endapo utashindwa kulipa kiasi kilichokopwa mara moja tutakutoza riba katika kiasi ambacho kimekopwa, kuanzia siku inayotakiwa kulipwa. Pamoja na tozo za riba, tutakutoza ada nyingine kama zinavyoanishwa katika jedwali la bei kadiri linavyorekebishwa na Benki mara kwa mara.

9.3 Tunaweza kudai malipo ya kiasi chote tunachokudai wakati wowote ule.

9.4 Cheti kinachotiwa saini na meneja wa Benki yetu kuonyesha undani wa kiasi chochote, pamoja na riba, unachodaiwa itakuwa uthibitisho wa kutosha mpaka inapothibitishwa vinginevyo.

9.5 Endapo itabidi tutachukua hatua za kisheria dhidi yako kwenye mahakama inayostahili.

9.6 Utawajibika kwa malipo ya gharama za maana katika kurejesha kiasi chochote tunachokudai, pamoja na gharama za kisheria kwa wakili na ufuatiliaji.

**10. Jumla**

10.1 Tunaweza kuhakikisha iwapo maelezo yako ya kina katika hati yako ya maombi ni sahihi na marejeo yoyote unayotupatia.

10.2 Sharti utuarifu mara moja endapo utawekwa chini ya amri ya kiutawala, kufilisiwa au kuwekwa chini ya aina yoyote ya ufilisi, zuio la kisheria, pamoja na msaada wa kibiashara.

## 1. Utangulizi

1.1 Hati hii ina Masharti kwa Bidhaa na Huduma zetu isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo katika Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma. Pamoja na Masharti haya kila Bidhaa na Huduma zetu zina maelezo na masharti ambayo ni mahsusi kwa Bidhaa/Huduma inayohusika (Masharti Maalum ya Bidhaa/Huduma).

**1.2 Masharti haya na Masharti Mahsusi mengine ya Bidhaa na Huduma yanafanya mkataba baina yako na sisi, kwa hiyo tafadhali hakikisha unayaelewa yote.**

**1.3 Ibara muhimu ambazo zinaweza kuondoa uwajibikaji wetu au zinahusu hatari zitaandikwa kwa wino mzito au msisitizo. Sharti uzingatie vizuri ibara hizi.**

1.4 Kumbuka kwamba siku zote sharti utimize Masharti haya.

## 2. Tafsiri

Tumetafsiri baadhi ya maneno kwa ajili ya usawa. Maneno haya yataanza na herufi kubwa, pale itakapoelezwa. Neno moja hujumlisha wingi na kinyume chake.

**Misimbo ya Matumizi:** Misimbo yoyote ya siri (herufi na tarakimu) unaotumia kupata Matumizi ya Bidhaa na Huduma Pamoja, kwa mfano: namba ya Kadi Yako, utambulisho wa kidigitali PINI, jina linalotumika na nywila inayotumika

**Akaunti:** Akaunti ya benki iliyofunguliwa na sisi kwa jina lako kwa maombi yako.

**Kadi ya Ziada:** Kadi yoyote ya ziada iliyounganishwa na Akaunti yako.

**Mmiliki ziada wa Kadi**: Mtu ambaye tunamkabidhi Kadi ya ziada baada ya maombi yako, mathalan mwenza, mshirika, mtoto au mfanyakazi

**Mkataba:**Fomu ya maombi iliyoambatanishwa na kusomwa pamoja na maelezo haya na Maelezo na Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma.

**ATM**: Mashine ya Kutoa Fedha Inayojiendesha.

**Siku ya Kazi**: Siku yoyote ambayo kwa kawaida kazi hufanyika katika Jamhuri ya Muungano Wa Tanzani ukiachia Jumamosi, Jumapili na Sikukuu za Umma.

**Biashara:** Mtu anayeomba kufungua Akaunti, au jina lake.

**Kadi:** Kadi yoyote ya Benki tunayotoa kwako kwa ajili ya Akaunti yako pamoja na Kadi ya Ziada au kadi mbadala.

**Msimbo:** ina maana ya Msimbo wa Hazina ya Marekani wa mwaka 1896 (kama unavyorekebishwa mara kwa mara).

**Makampuni**: Sheria ya Makampuni Na. 12 ya 2002 kama ilivyyo ilivyorekebishwa mara kwa mara pamoja na sheria za chini.

**Nyaraka Wezeshi:** Kama ilivyorejewa katika fomu ya maombi ambamo masharti haya yameambatishwa, ina maana,ikiwa ni kampuni, na kanuni za kampuni kuanzia biashara,cheti cha usajili na/au taarifa na cheti cha usajili kadiri iwavyo, au ikiwa ni shirika binafsi, taarifa ya kuanzishwa au ikiwa ni amana, hati ya amana na barua za mamlaka au ikiwa ni ushirika, mkataba na ushirika kama upo

**Ukomo wa EAP:** Ukomo wa malipo ya kielektroni ambao unaweza kuunganishwa na matumizi ya benki kwa intaneti kwenye benki izungukayo kwa ajili ya uhamishaji fedha kielektroni kutoka kwenye Akaunti yako

**FATCA:** ina maana ya Sheria ya Utekelezaji Kodi wa Akaunti za Kigeni za Marekani.

**Kundi:** Kundi la Benki ya Standard yenye ukomo wa madeni, tanzu zake na tanzu zake.

**HATI:** Kitu chochote kama vile kitabu cha hundi au kadi kwa ajili ya Matumizi ya Akaunti yako

**IRS:** ina maana ya Huduma ya Hazina ya Ndani ya Marekani (kadiri inavyorekebishwa mara kwa mara).

**Sheria:** Sheria, kanuni, hukumu, na amri za mahakama yoyote yenye mamlaka, Benki Kuu au wakala wa serikali au mamlaka yenye nguvu ya kisheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mamlaka yoyote inayohusika

**Mfanya biashara:** mtoaji bidhaa au huduma.

**Taasisi ya Fedha Isiyo Mshirika:** ina maana iliyoainishwa kwenye Msimbo

**Tumia:** Uendeshaji wa Akaunti yako, Utekelezaji na utendaji vina maana moja

**Taarifa Binafsi:** Taarifa kuhusu mtu halisi anayetambulika na au pale inabidi, mtu kisheria, pamoja na, lakini sio pekee, taarifa kuhusu mbari, jinsia, mimba, hadhi kindoa. utaifa, rangi, umri, hali ya kimwili au akili, uwezo kimali; athari, dini, imani, utamaduni, lugha, uzawa, elimu, kitabibu, kifedha; historia ya kijamii au ajira, namba yoyote ya utambuzi, alama, barua pepe, anuani ya posta au ya mahali, namba ya simu, eneo, kitambulisho chochote cha kimawasiliano; kazi nyingine yoyote ya mhusika; taarifa kuhusiana na Akaunti, maoni binafsi, maoni au utashi wa mhusika au maoni au utashi wa mtu mwingine mintarafu mhusika; mawasiliano yaliyotumwa na mhusika ambayo dhahiri au kiufahamifu yana silka ya kibinafsi au siri; au mawasiliano ya awali, na jina la mtu iwapo linawezekana kuwa na taarifa nyingine kuhusu mtu huyo au iwapo kufichuliwa kwa jina lenyewe kutaonyesha taarifa ya mtu huyo.

**PINI**: Namba ya siri ya utambulisho wa mtu inayotumika kwenye Akaunti yako, pamoja na PINI iliyochaguliwa na mteja.

**Mchakato:** Matumizi au kitendo chochote kinachojiendesha au la kuhusu Taarifa Binafsi, pamoja na: mabadiliko, uzuiaji, urekebishaji, ukusanyaji, ushauri, ushushaji, uharibifu, utoaji taarifa kwa njia ya usambazaji, au kufanya ipatikane kwa namna yoyote, ufutaji, uunganishaji, upangaji, upokeaji, kurekodi, kuchukua, kuhifadhi, kuboresha, kurekebisha au matumizi ya taarifa. **Utumiaji** na I**liyotumika** itakuwa na maana moja

**Bidhaa:** Aina mbalimbali za akaunti zisizo na miamala ya mikopo pamoja na akaunti za akiba na uwekezaji tunazozitoa kwa wateja wetu pamoja na huduma zinazohusiana na Akaunti. Huduma ina maana kama hiyo.

**Akaunti Hatarishi:** Ina maana ya Akaunti na Marekani ambayo haijatoa nyaraka zozote zilizotakiwa kuthibitisha umiliki wa mwenye Akaunti ya hadhi ya FATCA au daraja hilo.

**Kanuni:** Kanuni yoyote, amri ya kiofisi, maelekezo au muongozo (uwe na nguvu ya kisheria au la) au amri yoyote ambayo Benki imechagua na/au inawajibika kuitekeleza na/au iko kwa mujibu wa taratibu za benki yenye hadhi (katika upekee na hiari yake) ya serikali yoyote, serikali shirikishi, chombo cha kimataifa, wakala au idara au chombo cha udhibiti, mamlaka au shirika jingine.

**Mtu aliyezuiliwa:** Mtu (halisi au kisheria) ambaye amezuiliwa na Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo.

**Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo:** Moja au muungano wa asasi zifuatazo; Ofisi ya Udhibiti wa Mali za Kigeni za Idara ya Hazina ya Muungano wa Mataifa ya Marekani, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya, Hazina ya Malkia, Wizara ya Uchumi, Fedha na Viwanda ya Ufaransa na mamlaka inayotambuliwa na sisi mara kwa mara

**Benki ya Stanbic, Sisi**: Benki ya Stanbic Tanzania ( Namba ya Usajili 22443), Kampuni ya Marekani iliyosajiliwa rasmi kwa dhima ya ukomo kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Na.12 ya 2002, Tanzania Bara na kupewa leseni chini ya Sheria ya Taasisi za Benki na Fedha, 2006 (Sheria Na.5 ya 2006) kama ilivyorekebishwa na/au warithi wa mali au wahawilishiwa.

**Chanzo Mapato:** Ina maana ya mapato yasiyo badilika au yanayobadilika kwa mwaka au nyakati kutoka mapato ndani ya Marekani kama inavyoainishwa na FATCA, kanuni ya hazina ya marekani 1.1473- 1(a)(2). Wakala Mdhibiti maana yake ni taasisi ya fedha au benki yenye mamlaka ya kudhibiti Chanzo cha Mapato ya Marekani kwa mujibu wa mkataba na Marekani.

**Muamala:** Makato au nyongeza yoyote kwenye Akaunti yako yaliyofanywa iwe au isiwe Hati, PINI au kifaa kimetumika. Inajumlisha malipo yoyote ya bidhaa au huduma, kuweka, kutoa au kuhawilisha fedha au thamani. Fanya na Ufanyaji vina maana moja.

**US Muungano wa Mataifa ya Marekani, Akaunti ya Marekani**: Maana yake ni akaunti inayomilikiwa na raia wa Marekani, mlipa kodi mkazi wa Marekani au akaunti yenye mmiliki wa Marekani ambaye ni mtu aliyeainishwa na FATCA (Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa Akaunti za kigeni) Kanuni ya Hazina 1.1471.

**Wakala Mdhibiti:** Maana yake ni taasisi ya fedha au benki yenye mamlaka ya kudhibiti chanzo cha mapato cha Marekani kwa mujibu wa mkataba na Marekani.

**Wewe au Yako:** Ni mtu anayeomba kufungua Akaunti au ambaye Akaunti imefunguliwa kwa jina lake, pamoja na chombo cha kisheria

## 3. Uwasilishaj wa Hati na Uanzaji wa Kutumia Akaunti yako

3.1 Iwapo tutaidhinisha maombi yako unaweza Kuitumia Akaunti yako kwa mujibu wa Masharti haya ikiwa maelekezo mengine yoyote yametekelezwa. Tutakuarifu kuhusu masharti hayo.

3.2 Tunaweza kukukabidhi vifaa vya matumizi ya Akaunti yako unapoifungua.

3.3 Tutakuarifu wakati ambapo kifaa kitakuwepo au kitakuwa tayari kuchukuliwa katika tawi lako.

3.4 Utaweza tu kutumia Akaunti yako utakapochukua kifaa chochote kinachotakiwa kwa ajili hiyo.

3.5 Unaweza kurejesha kifaa chochote ambacho hakifanyi kazi vizuri wakati wowote na tutakibadilisha.

**4. Akaunti Yako**

4.1 Akaunti yako itahuishwa mara utakapoweka kiwango cha chini kinachotakiwa kufungua Akaunti.

4.2 Una wajibu kuhakikisha Akaunti yako inahuishwa.

4.3 Unaweza kuomba kuweka ukomo wa utoaji wa fedha kwa siku au mwezi.

4.4 Hutaweza kutumia Akaunti yako kwa ajili ya kukinufaisha moja kwa moja au vinginevyo chombo kilichodhibitiwa.

4.5 Endapo tutashuku kwamba Akaunti yako imetumika kwa wizi, kizembe, kinyume na sheria, shughuli za utakatishaji pesa au kugharamia ugaidi na vitendo vinavyohusika nao, tunaweza:

4.5.1 kuzuia matumizi kwenye; au

4.5.2 kusitisha matumizi ya Akaunti yako mara moja bila taarifa kwako.

**5. Maelezo kwenye Akaunti yako**

5.1 Unaweza kutuomba maelezo ya Akaunti yako muda wowote katika tawi letu lolote na jukwaa la mtandao wa kielektroni.

5.2 Ikiwa unaamini kuna makosa katika maelezo ya Akaunti yako sharti utuandikie au utembelee tawi lako ndani ya siku thelathini (30) ya tarehe ya maelezo yenyewe.

5.3 Ikiwa hutatueleza kuhusu makosa yoyote ndani ya siku hizi thelathini (30) tutachukulia kwamba maelezo ya Akaunti yako ni sahihi.

**6. Utumiaji wa Kadi yako**

**6.1 Masharti ya Jumla ya Kadi**

6.1.1 Sharti utie saini Kadi zako kwa wino wa kudumu unapozipokea. Tumia nafasi nyuma ya Kadi yako.

6.1.2 Kadi hazitatumiwa kwa shughuli zozote haramu.

6.1.3 Daima utakuwa ndio mmiliki wa Kadi hizi.

6.1.4 Endapo utapoteza Kadi yako sharti ulipie mpya.

6.1.5 Sharti utumie Kadi mwenyewe.

6.1.6 Huruhusiwi kuhawilisha Kadi yako kwa mtu mwingine yeyote.

6.1.7 Tutakupa PINI kukuwezesha kutumia Kadi yako.

6.1.8 Sharti ufuate kanuni za ubadilishaji pesa unapofanya miamala nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6.1.9 Unaweza kutumia Kadi katika ATM yoyote, na kwa ajili ya miamala mingine, unaweza kutumia Kadi yako katika ATM ambazo sio za Stanbic lakini utalipia ada ya ziada kwa kutumia mashine hizo.

**6.2 Uwekaji pesa katika ATM na utoaji pesa ulizoweka**

6.2.1 Unaweza kuweka pesa kwenye ATM za Stanbic pekee.

6.2.2 Pesa uliyoweka kwenye ATM ya Stanbic yoyote itajionyesha mara moja katika Akaunti yako.

6.2.3 Akaunti yako itawekewa ukomo wa utoaji pesa kwa siku. Unaweza kubadilisha hilo kwa kuomba kupitia mitandao ya huduma ya Benki ya Stanbic, pamoja na, ingawa sio pekee, kupitia benki yetu kwa intaneti au kupitia huduma ya Benki kwa simu. Unaweza kupunguza kima hicho kwa kutumia mtandao wowote.

**6.3 Miamala ya Kadi ya Utoaji**

6.3.1 Unaweza kutumia Kadi yako ya utoaji kufanya uingize kwa Mfanyabiashara yeyote atakayeikubali.

6.3.2 Unapofanya muamala wa Kadi ya Utoaji sharti uingize PINI yako au tia saini hati ya muamala au vyote.

6.3.3 Hutatumia Kadi ya utoaji kwa miamala ya mbali kama kuweka ada kwa barua, simu au Intaneti.

**6.4 Kadi za Ziada**

6.4.1 Tunaweza kutoa Kadi za Ziada kwenye Akaunti yako iwapo utaomba. Masharti haya yanatumika kwenye Kadi za Ziada na Mmiliki kadi ya Ziada yeyote sharti akubaliane na Masharti haya kabla ya kukabidhiwa Kadi ya Ziada.

**6.4.2 Ama wewe au Mmiliki wa Kadi ya Ziada mnawajibika kwa kiwango chote kwenye Kadi yako ya Ziada au tunaweza kujilipa kiwango chote kutoka kwenu kwa namna ambayo tutaamua. Kisheria hii inarejewa kama uwajibikaji wa pamoja na pekee.**

**6.5 Usalama na upoteaji au kadi zilizoibwa**

**6.5.1 Sharti muda wote uwe makini na Kadi yako na Misimbo ya Utumiaji kwa sababu wizi wa vitambulisho vya kibenki ni jambo linalotokea mara nyingi na kukua mathalani barua pepe, tovuti, simu, taarifa fupi (sms) za udanganyifu.**

**6.5.2 Unawajibika kwa uwekaji na matumizi mazuri ya Kadi zako. Usitoe Misimbo ya Utumiaji kwa yeyote. Sharti ukariri Misimbo ya Utumiaji yako au uiweke mahali salama mbali na Kadi yako.**

**6.5.3 Ikiwa utadharau usalama wa Kadi yako au Misimbo ya utumiaji kuna hatari mtu mwingine anaweza kuitumia na/au kufanya muamala kwenye Akaunti yako. Mtu mwingine anaweza kutumia Kadi yako kwa wizi na/au misimbo ya utumiaji kuomba na/au kusajili huduma mpya kama vile benki ya kielektroni, benki ya mtandao, benki ya simu ya kiganjani, au benki ya simu. Hii itaruhusu watu wengine kufanya, kwa mfano kuomba mkopo, kuomba nyongeza ya ukomo wa mkopo na mabadiliko ya uwezeshaji, ukomo wa mkopo, ukomo wa ATM au ukomo wa EAP. Vitendo hivyo vya udanganyifu vinaweza kufanywa kupitia mitandao mbalimbali ya huduma za kibenki, pamoja na lakini sio pekee, ATM; pia huduma zetu za benki kielektroni kwa**

**kutumia vifaa kama simu za viganjani, kompyuta, kompyuta mpakato n.k.**

**6.5.4 Ikiwa tutapokea maelekezo kutoka kwako, kwa kutumia Misimbo ya Utumiaji, hatuwajibiki kuhakiki ukweli wa maelekezo hayo na hii itakuwa hivyo pia iwapo maelekezo ni ya udanganyifu, isipokuwa tu itakapothibitika kwamba tulijua dhahiri kuwa maelekezo yalikuwa ya udanganyifu.**

**6.5.5 Sharti utuarifu mara moja ikiwa unagundua kwamba Kadi au Misimbo ya Utumiaji vimepotea, kuibwa au kuingiliwa. Tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuzuia Kadi mara unapotuarifu.**

**6.5.6 Kadi inapozuiliwa haitaweza tena kutumika. Hata hivyo mitandao ya huduma zetu za kielektroni mtu yeyote anaweza kuangalia au kufanya muamala kwenye Akaunti nyingine zozote kwa vile hizi zote zimeunganishwa na Kadi yako. Iwapo utataka akaunti nyingine zipatikane na kutumika kwenye mitandao mingine sharti utuarifu kufanya hivi na utafanya hivyo kwa uthubutu wako mwenyewe.**

6.5.7 Utawajibika kwa Miamala ya Kadi yote mpaka unapotuarifu kwamba Kadi yako au Misimbo ya Utumiaji imepotea, ibwa au kuhatarishwa.

**6.6 Kutayarisha Malipo ya Kadi**

6.6.1 Tutatoza Akaunti yako kwa malipo tunayoyafanya kwa niaba yako kuhusiana na Miamala ya Kadi.

**6.6.2 Mgogoro wowote baina yako na Mfanyabiashara hautaathiri haki yetu ya kulipwa na wewe. Hatutawajibika kwa hasara yoyote au gharama kuhusiana na mgogoro.**

6.6.3 Sharti utatue mgogoro baina yako na Mfanyabiashara kwa vile hatutahusika. Usizuie Muamala wa Kadi wowote. Unaweza ukahoji Muamala wa Kadi lakini sharti uthibitishe kwamba haukuidhinishwa na wewe kabisa.

6.6.4 Huwezi kusitisha Muamala wa Kadi wowote. Unaweza kupinga Muamala wa Kadi lakini sharti uthibitishe kuwa haukuruhusiwa kabisa.

## 7. Ada, riba, ukomo na upangaji bei

7.1 Taarifa kuhusu tozo (ada, kodi, faini na kadhalika) ambazo tunatumia kuhusu Bidhaa na Huduma zetu zinazoonyeshwa kwenye jedwali letu la ada ambayo iko kwenye kijarida cha uwekaji bei ambacho hukichapisha, ni halali na inatumika kuanzia Januari 1 hadi Desemba 31 kila mwaka, isipokuwa tutakapowasiliana vinginevyo.

7.2 Kijarida chetu kipya unaweza kukipata kutoka tawi letu lolote, au kutoka tovuti www.stanbicbank.co.tz.

7.3 Tunaweza kuzipitia gharama zetu kulingana na mzunguko wa mapitio wa mwaka au wakati wowote kwa hiari yetu.

7.4 Tutakutoza ada ya ziada kwa kutumia ATM ambayo sio ya Benki ya Stanbic.

7.5 Viwango vyote vya riba vinawekwa kwa mwaka.

7.6 Hatutakutoza riba zaidi ya ile inayoruhusiwa na sheria.

7.7 Pale ambapo riba inalipwa na sisi kwako itakokotolewa kutokana na bakaa la kila siku katika Akaunti yako na kulipwa kila mwezi au vinginevyo, kama tutakavyoridhia, isipokuwa kwa Akaunti za akiba, riba itakayolipwa na sisi itakatwa kodi inayotumika.

7.8 Hatutakulipa riba katika akaunti yoyote mpaka malipo hayo yawe yameelezwa kama sehemu ya Huduma inayohusika. Kwa mujibu wa Masharti yetu maalum ya Bidhaa ya Huduma tunaweza kubadilisha viwango vya riba tutakavyokulipa kwa hiari yetu na mabadiliko yoyote yanaweza kutumika baada ya taarifa ya siku thelathini (30).

7.9 Utawajibika kwa ada, tozo, kodi na riba zote tunazokuletea kwa mujibu wa Masharti haya na kijarida kipya kila inapostahili pamoja na gharama za kufidia madeni tunayokudai. Hii inajumlisha ada za kisheria kwa kiwango cha wakili na mteja, gharama za ukusanyaji na ada za ufuatiliaji.

## 8. Hifadhi ya Data

8.1 Unaridhia kwetu kukusanya Taarifa yako Binafsi kutoka kwako na inapokuwa halali na inafaa, kutoka vyanzo vya umma kuhusu mikopo, udanganyifu na madhumuni ya utekelezaji pamoja na madhumuni yaliyoainishwa hapa chini.

8.2 Endapo utatupa Taarifa Binafsi kuhusu au kwa niaba ya mtu mwingine ( pamoja na, ingawa sio pekee, watia saini akaunti, wenyehisa, wadhamini na wanufaishwa) unathibitisha kuwa unaruhusiwa (a) kutupa Taarifa Binafsi, (b) kuridhia kwa niaba yao kwa utumiaji wa Taarifa zao Binafsi hususan Utumiaji wa Taarifa Binafsi ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinakotolewa; na (c) kupokea taarifa zozote za siri kwa niaba yao.

8.3 Unaridhia kwetu kutumia Taarifa yako Binafsi:

8.3.1 kukupa bidhaa na huduma kwa mujibu wa mkataba huu wa bidhaa na huduma nyingine ambazo unaweza kuomba;

8.3.2 kufanya utafiti wa takwimu na mwingine kuainisha masoko mapya na mwenendo wake, kutathmini na kuboresha biashara yetu (hii inajumlisha kuboresha na kuendeleza bidhaa na huduma mpya);

8.3.3 kwenye nchi za nje ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Nchi hizi zinaweza zisiwe na sheria za hifadhi sawa na zile za nchi ambako bidhaa na huduma hutolewa. Tunapoweza tutamuomba mpokeaji kuridhia sera zetu binafsi;

8.3.4 kwa kutumia Taarifa yako Binafsi na watoaji wetu wa huduma na wakataji bima ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma hutolewa. Tunawaomba watu wanaotoa huduma kwetu, pamoja na wakataji bima, kuafikiana na sera zetu binafsi ikiwa wanahitaji kutumia Taarifa Binafsi yoyote kutekeleza majukumu yao; na

8.3.5 ndani ya Kundi.

8.3.6 Unatambua kuwa tunatakiwa na sheria mbalimbali kukusanya sehemu ya Taarifa yako Binafsi na unaridhia kutumia taarifa hii na sisi.

8.4 Utapata taratibu za Utumiaji wetu katika maelezo ya Kundi na yetu binafsi. Maelezo haya yanapatikana katika tovuti ya Kundi au kwa maombi.

8.5 Ikiwa huna hakika na hali yako ya Kodi au kisheria kwa kuwa Taarifa yako Binafsi inatumika katika nchi mbali na unayoishi, pata ushauri binafsi.

**8.6 Utafutaji Masoko**

8.6.1 Hapa unaridhia kwa Benki kutumia data na taarifa yako binafsi ndani ya kundi iwapo ni lazima kwa madhumuni ya utafutaji masoko na utoaji huduma kwako.

8.6.2 Tunaweza kutumia Taarifa yako Binafsi kukueleza kuhusu bidhaa, huduma na ofa maalum kutoka kwetu au kampuni ambazo zinaweza kukuvutia. Tutafanya hivi kupitia baruapepe, ujumbe wa maandishi (sms) , mitandao ya jamii au kukuarifu kwenye maombi yako ya simu ya kiganjani. Iwapo baadaye unaona hutaki sisi kufanya hivi, tafadhali wasiliana nasi kupitia mtandao wetu wa huduma kwa wateja kusitisha huduma hii.

**9. Utambulisho na udhibiti kuhusiana na udanganyifu**

Tunaweza kufanya utambulisho na udhibiti kuhusiana na udanganyifu kwako na kubadilisha taarifa kuhusiana na maombi yako kwako mintarafu Akaunti yako na uendeshaji wa Akaunti yako kwa jumla na mamlaka husika

**10. Kubadilishana taarifa kuhusu tuhuma za mwenendo wa kihalifu**

Iwapo tunashuku kwamba Akaunti yako inatumika kwa shughuli za kihalifu, tunaweza pia kutoa taarifa za undani kuhusu Akaunti na mawasiliano yako pamoja na undani wa mwenendo wa Akaunti yako vilivyosababisha tuhuma yetu kwa mamlaka husika.

**11. Mikopo na udhibiti husika**

Tunaweza kuchunguza kuhusu hali yako ya kifedha wakati wowote na sharti utupatie taarifa yoyote ya kifedha au taarifa muhimu ambayo tunaweza kuiulizia mara kwa mara.

11.1 Tunaweza kuchunguza mwenendo wako wa mkopo na mawakala wa taarifa na mikopo wowote au mhusika yeyote.

11.2 Tunaweza kuwapatia mawakala wa taarifa za mikopo taarifa sahihi kuhusu uendeshaji wa Akaunti yako pamoja na kushindwa kwako kutekeleza masharti haya.

11.3 Tunaweza kuzipatia benki nyingine, baada ya kuombwa, taarifa za benki kuhusu mwenendo wa Akaunti yako.

**12. Kukatisha uhusiano wako na sisi**

12.1 Huwezi kuachia au kuhamisha haki zako zozote au wajibu katika Mkataba huu bila idhini yetu ya maandishi kwanza.

12.2 Ikiwa umeamua kufunga Akaunti yako sharti uende kwenye tawi lako na ithibati ya utambulisho wako.

12.3 Ikiwa unafunga Akaunti yako sharti iwe imefuata sheria zote kabla ya kutoa pesa kutoka Akaunti hiyo.

12.4 Tunaweza kufunga Akaunti yako kwa kutoa kwako taarifa ya maandishi ya siku thelathini (30).

12.5 Hatuhitaji kukupa taarifa katika mazingira yafuatayo na tunaweza kufunga Akaunti yako mara moja katika mazingira yafuatayo, iwapo:

12.5.1 tunaamini au kushuku kwamba inatumika kiudanganyifu, kizembe, kinyume na sheria, au kwa shughuli za utakatishaji pesa, au kufadhili shughuli za kigaidi au zinazohusiana nazo;

12.5.2 tunaamini au kushuku kwamba Utumiaji wa Akaunti yako moja kwa moja au vinginevyo unanufaisha Chombo Kilichozuiwa;

12.5.3 tunaarifiwa kuwa ni Chombo Kilichozuiwa; au

12.5.4 sharti tufanye hivi kwa sababu nyingine za kisheria.

12.6 Ikiwa tutafunga Akaunti yako tunaweza kudai pesa yoyote tunayokudai. Sharti ulipe fedha zote tunazokudai kwa mujibu wa tarehe ambayo kwenye Taarifa ya Ukatishaji.

12.7 Tutakuarifu kwa maandishi kupitia mitandao yetu mbalimbali iwapo tunaamini kwamba hutumii tena Akaunti yako. Tutakupa fursa ya kuanza kutumia Akaunti yako tena ambapo tunaweza kuifunga endapo hutaanza kuitumia tena.

12.8 Ikiwa Akaunti yako imefungwa sharti ufanye yafuatayo mara moja:

12.8.1 kata Kadi yako katika vipande vipande ili isiweze kutumika tena. Iwapo hutaikata Kadi yako utawajibika kwa Miamala yote ya Kadi baada ya kufungwa kwa Akaunti yako; na

12.8.2 haribu hundi zote ambazo hazijatumika ili zisiweze kutumika tena. Ikiwa hutaharibu hundi ambazo hazikutumiwa hatutawajibika kwa upoteaji au hasara anayoipata mtu yeyote iwapo hundi hizi zitatumika kwa udanganyifu.

**13. Anuani za Taarifa**

13.1 Anuani ya mtaa wako kwenye fomu ya maombi ndio anuani uliyochagua kwa kupokelea taarifa na hati zozote za kisheria. Sharti utuandikie mara moja iwapo anuani yako itabadilika.

13.2 Tunaweza kuamua kutunza taarifa ambazo sio za kisheria kuhusiana na Akaunti yako kwenye anuani ya barua pepe yako, kama ipo, unayoitoa kwenye fomu ya maombi au kwenye anuani ya posta unayoitoa kwenye fomu ya maombi yako.

13.3 Tutachukulia kuwa umepokea taarifa yoyote tunayoituma kwako ndani ya siku kumi na nne baada ya kuposti, au siku ile ile iwapo itatumwa kwa mkono au kwa barua pepe.

13.4 Sharti utuarifu mara moja kuhusu mabadiliko yoyote ya anuani.

13.5 Tunachagua kuwa anuani yetu kwa ajili ya mienendo ya taarifa za kisheria ambapo michakato na taarifa zinazohusiana au kutokana na Mkataba huu, ukiukaji au uvunjwaji wake inaweza kutumwa au kuletwa kwetu, kama:

Benki ya Stanbic Tanzania
Kiwanja Na. 99
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/Barabara ya Kinondoni
SLP 72647
Dar es Salaam

## 14. Utekelezaji

14.1 Tunatakiwa na sheria kuomba taarifa fulani kukuhusu na watu wengine wanaokuhusu au kuhusiana na wewe na kuhakikisha taarifa hiyo na nyaraka ambazo tutaomba kutoka kwako ikiwa tutaamini ni muhimu au sahihi.

14.2 Ikiwa hutatekeleza maombi yetu au ukiwa hutupi taarifa au nyaraka tunaweza kukataa maombi yoyote uliyoyaleta kwetu au tunaweza kufunga Akaunti yako mara moja.

14.3 Ikiwa wakati wowote tunashuku kuwa Akaunti yako hailingani na sheria, tunaweza kuzuia miamala kuanzishwa au kutekelezwa mpaka Akaunti yako ifuate sheria kikamilifu.

## 15. Jumla

15.1 Tunaweza kubadilisha Masharti haya wakati wowote kwa kutoa taarifa ya maandishi kwako. Mabadiliko hayatakatisha mkataba huu.

15.2 Huwezi kubadilisha vipengele vyovyote vya Masharti haya.

15.3 Masharti maalumu ya Bidhaa/Huduma yatatumika iwapo kuna mgongano baina yake na Masharti ya waraka huu. Masharti haya yanasimamiwa na Sheria ya Tanzania.

15.4 Tunaweza kukushtaki katika mahakama yenye mamlaka rasmi.

15.5 Upendeleo au nafuu tunayoweza kukuruhusu havitaathiri au kubadilisha haki zetu zozote dhidi yako.

15.6 Iwapo unatudai fedha, hati iliyotiwa saini na meneja wetu yeyote kueleza kwamba:

15.6.1 ukweli kwamba deni linatakiwa kulipwa;

15.6.2 kiasi cha kulipwa;

15.6.3 riba inayohusika; na

15.6.4 tarehe ya kuanzia kukokotoa riba, itakuwa ni uthibitisho tosha wa maelezo yaliyotolewa kwenye hati, isipokuwa unapoweza kuthibitisha vinginevyo. Sio lazima kuthibitisha kuajiriwa kwa meneja aliyetia saini hati.

15.7 Lazima utuandikie mara moja endapo mazingira yako yanabadilika au yanaweza kusababisha hatari kwetu.

15.8 Kutotumika, ubatili au kutotekelezeka kwa ibara yoyote ya Masharti haya maalumu ya Bidhaa/Huduma hakutaathiri utumikaji, uhalali au utekelezaji wa ibara nyingine za Masharti haya au Masharti Maalum ya Bidhaa/Huduma yoyote.

## 16. Kuondolewa kwa majukumu yetu kwako

16.1 Sisi (pamoja na mtu yeyote ambaye tunawajibika kwake) hatutawajibika kwa hasara yoyote (pamoja na zile zilizoelezwa katika ibara ya 17.2 hapa chini) kutokana na:

16.1.1 kufungwa kwa au kusitishwa matumizi kwa au kuzuiwa kwa shughuli zozote kwenye Akaunti yako na sisi kwa sababu yoyote;

16.1.2 kutekeleza kwetu sheria zozote;

16.1.3 mazingira yoyote nje ya uwezo wetu kama vile (bila ukomo) majanga ya asili yasiyozuilika katika utendaji, migomo, au migogoro ya kikazi, vurugu, ghasia za kiraia au fujo, makatazo yoyote yaliyowekwa ( au hatua iliyochukuliwa) na Mamlaka ya Uwekezaji Vikwazo, mamlaka ya kiserikali au ksiheria au mtu mwingine yeyote; kuingiliwa kokote kwa Huduma, ucheleweshaji, kukatika kwa umeme, kuharibika kwa kifaa chochote, kituo cha data za kielektroni, ATM, mtandao au mfumo mwingine.

16.2 Masharti ya ibara ya 16.1 yanajumlisha madai kwenye mkataba, tendo au sheria kwa adhabu dhahiri au la ; hasara inayosababishwa au mahususi pamoja na ukosaji wa faida.

## 17. Kuondolewa kwa majukumu yetu kwako

17.1 Sisi (pamoja na mtu yeyote ambaye tunawajibika kwake) hatutawajibika kwa hasara yoyote (pamoja na zile zilizoelezwa katika ibara ya 17.2 hapa chini) kutokana na:

17.1.1 kufungwa kwa au kusitishwa matumizi kwa au kuzuiwa kwa shughuli zozote kwenye Akaunti yako na sisi kwa sababu yoyote;

17.1.2 kutekeleza kwetu sheria zozote;

17.1.3 mazingira yoyote nje ya uwezo wetu kama vile (bila ukomo) majanga ya asili yasiyozuilika katika utendaji, migomo, au migogoro ya kikazi, vurugu, ghasia za kiraia au fujo, makatazo yoyote yaliyowekwa ( au hatua iliyochukuliwa) na Mamlaka ya Uwekezaji Vikwazo, mamlaka ya kiserikali au ksiheria au mtu mwingine yeyote; kuingiliwa kokote kwa Huduma, ucheleweshaji, kukatika kwa umeme, kuharibika kwa kifaa chochote, kituo cha data za kielektroni, ATM, mtandao au mfumo mwingine. Tutakuarifu mapema kupitia njia mbalimbali, hii ni pamoja lakini sio pekee, ujumbe mfupi wa simu, barua pepe, barua, taarifa kwenye ATM, kwenye matawi yetu na njia nyingine ambazo tutaona muhimu mara kwa mara.

17.2 Masharti ya ibara ya 17.1 yanajumlisha madai kwenye mkataba, tendo au sheria kwa adhabu dhahiri au la; hasara inayosababishwa au mahususi pamoja na ukosaji wa faida.

## 18. Sheria ya Utekelezaji wa Akaunti za Kigeni

18.1 Unaelewa kuwa kama sehemu ya majukumu ya Benki kutekeleza FATCA, tunatakiwa kupata taarifa kuhusiana na kodi yako kuamua iwapo Akaunti yako ni ya Marekani, Akaunti ya Mmiliki Mkorofi au Taasisi ya Fedha ya Kigeni isio Mshirika.

18.2 Unaipa Benki ridhaa ya:

18.2.1 kupata kutoka kwako taarifa kuhusu kodi kadiri inavyohitajika na katika muundo ulioamuliwa na Benki kuamua iwapo unaangukia katika kundi lolote la hapo juu, ambapo data za asili yako na miamala mtambuka kama inavyoamuliwa mara kwa mara na US IRS, itawasilishwa na Benki kwa IRS;

18.2.2 kwa Mawakala wa Uzuiaji ikiwa na wakati itatakiwa chini ya kanuni za FATCA; kuzuia malipo yoyote ya vyanzo vya Mapato ya Marekani yaliyopokelewa na wewe kwa kiwango ambacho hakijawahi kufanywa na Wakala wa Uzuiaji yeyote (zingatia kwamba

uzuiaji wa juu unaoweza kutumika kwa vyanzo vya mapato vya Marekani chini FACTA ni asilimia 30); na

18.2.3 kufunga, kuzuia au kuhamisha (kwa moja ya vyombo vyetu maombi vinavyohusika) Akaunti yako ndani ya siku tisini (90) kwa taarifa yangu kuhusiana na kodi (kwa muundo utakaoamuliwa na sisi).

**19. Malalamiko ya Wateja**

19.1Ili kuifanya iwe rahisi kadiri inavyowezekana zifuatazo ni njia za kutuma malalamiko yako kuhakikisha kwamba yamesikilizwa:

19.1.1 Tembelea moja ya Benki zetu na kuzungumza na mfanyakazi wake;

19.1.2 Tuma malalamiko yako kwa mtandao kwa: tanzaniaccc@stanbic.co.tz;

19.1.3 Piga Kituo cha Kuwasiliana na Wateja laini ya bure **Na. 0800 751111** au; 19.1.4 . Weka malalamiko yako kwa maandishi na tuma kwa:

Meneja CCC
Benki ya Stanbic
Makao Makuu
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/Barabara ya Kinondoni
SLP 72647
Dar es Salaam

19.2 Endapo malalamiko yako hayatatatuliwa ndani ya siku ishirini na moja (21) (au muda uliokubaliwa) au iwapo hukuridhika na matokeo ya mchakato ulioanishwa na ibara ya 19.1 hapo juu, unaweza kupeka malalamiko mbali zaidi kwa kutuma barua pepe kwa tanzaniaservice@stanbic.com au andika kwa:

**Mkuu wa Huduma**
Benki ya Stanbic
Makao Makuu
Kona ya Ali hassan Mwinyi/ Barabara ya Kinondoni
S.L.P 72642
Dar es Salaam

19.3 Endapo itatokea bado hujaridhika na utatuzi wetu unaweza kupeleka malalamiko yako kwa maandishi kwenye dawati la malalamiko la Benki Kuu ya Tanzania:

Dawati la Kutatua Malalamiko
Ofisi ya Katibu wa Benki
2 Mtaa wa Mirambo
SLP 11884
Dar es Salaam